

**Swahili transcript:**

Nchi ya Tanzania pia imepiga hatua kubwa sana ya kimaendeleo japo ni nchi ambayo inaendelea, lakini katika hali halisi kwa sasa imepiga hatua kubwa sana katika suala zima la maendeleo. Nikizungumzia kwa suala la elimu, kwa sasa Tanzania tuna shule nyingi sana za msingi, serikali iliweka mkakati wa kuanzisha shule nyingi za msingi ili kuwawezesha watanzania wengi na hasa waishio vijijini kuweza kupata elimu hii ya msingi. Vilevile kuna shule nyingi za sekondari ambazo zimeanzishwa hivi karibuni, sekondari za serikali na sekondari za watu binafsi. Kwa hiyo watanzania wengi wanapata fursa ya kwenda shule, wengi wanakwenda shule sasa tofauti na ilivyokuwa kipindi cha nyuma kidogo kwamba shule zilikuwa ni chache na wachache waliweza kwenda kupata elimu, lakini kwa sasa watanzania wengi wamenufaika na elimu ya msingi na vilevile elimu ya sekondari. Na nikizungumzia kuhusu elimu ya juu ya chuo kikuu, kwamba kwa sasa tumepiga hatua kubwa sana, tuna vyuo vikuu vingi nchini tofauti na ilivyokuwa zamani, zamani tulikuwa na chuo kikuu cha Dar es salaam, lakini katika miaka ya hivi karibuni vimeanzishwa na vyuo vikuu vingine ambavyo hutoa fursa kwa wanafunzi wanapomaliza aah! elimu ya sekondari na wanapoenda high school wanajiandaa kuingia chuo kikuu, kwa hiyo imewapa changamoto kubwa sana hasa wanafunzi ambao wanamaliza na wanajiandaa kuingia chuo kikuu kwamba kwa sasa tuna vyuo vikuu vingi. Tuna chuo kikuu cha Sokoine ambacho kipo mkoa wa Morogoro, tuna chuo kikuu cha Tumaini ambacho kipo mkoa wa Iringa, tuna chuo kikuu cha Augustine ambacho kipo mkoa wa Mwanza, tuna chuo kikuu cha usanifu wa majengo ambacho kipo mkoa wa Dar es salaam, tuna chuo cha usimamizi wa fedha ambacho kipo mkoa wa Dar es salaam, na kuna chuo kikuu cha Muhimbili ambacho kipo mkoa wa Dar es salaam na vyuo vikuu vingine vingi ambavyo bado sijavitaja. Kwa hiyo katika kipindi hiki imekuwa ni changamoto kubwa kwa watanzania wengi, na watanzania wengi wanapata nafasi ya kwenda kusoma katika vyuo vikuu ambavyo viko katika nchi yetu ya Tanzania.

### **English translation:**

The country of Tanzania has made a step forward in development although it is still in the process of developing. But in a real sense, at present it has made a big step in its development. I am talking about education. Now in Tanzania we have many primary schools. The government made a deal to establish more primary schools to enable Tanzanians, especially in rural areas, to have an opportunity for education. Also we have many secondary schools which have been established recently. They include government and private secondary schools. So many Tanzanians have the opportunity to get an education. Many more are going to school now when compared to how it was in the past. In the past, schools were few and just a few people went to school, but now many Tanzanians have the opportunity to have primary and secondary education.

As for higher education, we have also made much progress. We have many universities compared to how it was in the past. In the past, we had the University of Dar es Salaam. But in recent years, many universities have been established. So now students who finish high school have the opportunity to enroll in a university. That gives them a big incentive to do well in high school because after that they know that they will have a chance to enroll in a university. We now have many universities such as Sokoine University in Morogoro and we have Tumaini University in Iringa and Augustine University in Mwanza. We also have the University College of Lands and Architectural Studies in Dar es Salaam and the Institute of Finance Management in Dar es Salaam. There is Muhimbili University in Dar es Salaam and other universities which I have not yet mentioned. So at this time, there is a big incentive for many Tanzanians to have the opportunity to study at these universities which are in our country, Tanzania.

**About CultureTalk:** CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.